April 1, 2021 Uk.5, Habari Leo

# Ugonjwa wa ngozi wa ng'ombe waibua hofu Mpwapwa

**Na Sifa Lubasi, Mpwapwa**

BAADHI ya wafugaji wilayani Mpwapwa mkoani Dodoma wameingiwa hofu baada kupoteza mifugo yao kutokana na kuzuka kwa ugonjwa wa ngozi kwa ng'ombe ujulikanao kitaalamu kama 'Lamp Skin Diseaces' ambao husababisha ng'ombe kutokwa vipele.

Mmoja wa wafugaji hao, Pastory Shisewo alisema ugonjwa huo umeshaua ng'ombe wengi na baadhi ya wafugaji wamepoteza zizi zima kutokana na ng'ombe wao kufa. Alisema bado hawajapata maelezo kutoka kwa wataalamu wa mifugo ngazi ya kata na wilaya kwa kuwa hawajawatembelea na kueleza kuwa wanahitaji ushauri kuhusu nini wafanye na namna ya kuitibu mifugo yao.

Mfugaji mwingine, Tabitha Simbeya alisema katika mtaa wake zaidi ya mazizi 10 yameathiriwa na ugonjwa huo unaosababisha ng'ombe kuvimba ngozi na kushindwa kula vizuri, kukonda na hatimae kufa.

Ofisa Mifugo na Uvuvi Wilaya ya Mpwapwa, Godfrey Ayako amethibitisha kuwapo kwa ugonjwa huo katika wilaya hiyo na kueleza kuwa unatokana na virusi na hauna tiba bali kinachotakiwa ni mfugo kupatiwa chanjo.


Alisema ugonjwa huo huenea kwa kasi kutokana na wafugaji kuchanganya makundi ya ng'ombe katika malisho na kusababisha waambukizane.

Aliwataka wafugaji kujiunga kwenye vikundi ili kuzikabili changamoto za mifugo ikiwamo kuwapatia chanjo wanyama wao na matibabu pindi ugonjwa unapotokea.

"Ugonjwa huu hauna tiba, hivyo kinga ndiyo njia pekee ya kuuzuia usiwapate mifugo yako na kinga pekee ni kutumia chanjo, hivyo chanja mifugo yako kabla ugonjwa haujaingia maana ukishaingia huruhusiwi kuchanja hadi pale utakapotokomea," alisema.

Mmoja wa watafiti wa mifugo kutokaTasisi ya Utafiti wa Mifugo (Tarili) Mpwapwa ambaye hakutaka jina lake liandikwe, alisema ugonjwa huo ni hatari kwa mifugo na hutokea kwa msimu, hivyo idara ya mifugo na uvuvi inatakiwa kutoa elimu kwa wafugaji jinsi ya kuepukana na ugonjwa ili kuepuka hasara kutokana na mifugo kufa.

Scanned with CamScanner



Alhamisi Aprili 1, 2021 Nipashe 15

# Uvuvi bahari kuu kuboreshwa kwa kujenga bandari ya uvuvi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema kuwa katika bajeti ya sekta ya uvuvi ya mwaka 2021/22 imepanga kuboresha shughuli za uvuvi wa bahari kuu nchini na inatarajia kuanza ujenzi wa bandari ya uvuvi itakayo saidia kuongeza mapato yataokanayo na mazao hayo.

Katika bajeti hiyo Sh. bilioni 50 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa bandari hiyo.

Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia sekta ya uvuvi, Dk. Rashid Tamatama, aliyasema hayo juzi wakati alipokuwa akiwasilisha bajeti ya wizara hiyo mbele ya Kamati ya Bunge ya Mifugo, Maji na Kilimo.

Alisema, katika bajeti hiyo maeneo ya vipaumbele ni pamoja na ujenzi wa bandari ya uvuvi itakayojengwa ili kuongeza ufanisi katika sekta hiyo nchini.

Dk. Tamatama, alisema kuwa hivi sasa mchakato wa kujenga bandari hiyo ya uvuvi upo katika hatua za kiuandaaji wa michoro na baada ya kukamilika hatua nyingine itafuata.

"Ili kuboresha shughuli hizi za uvuvi kuwa na tija na kuongeza pato la taifa kupitia sekta hii lazima tujenge bandari ya uvuvi itakayosaidia kuongeza uvunaji wa samaki tofauti na ilivyosasa na katika bajeti yetu hii tumetenga Sh. bilioni 50, kwa ajili ya ujenzi huo," alisema Dk. Tamatama.

Pia alisema lengo la serikali ni kuhakikisha kuwa inafufua shirika la uvuvi nchini ili kusimamia shughuli za uvuvi.

"Tunapanga kununua meli za uvuvi ambazo zitakuwa chini ya shilirika hilo la uvuvi na tunatarajia hadi Desemba mwaka huu au Januari mwakani, tutakuwa tumenunua meli ya uvuvi ya kisasa yenye vifaa vyote," alisema.

Alisema kuwa kupitia ufadhili wa nchi ya Japani tayari meli hiyo imeshaanza kujengwa katika nchi ya Srilanka na hadi Januari mwakani wanatarajia kuwa iwe imefika nchini na kuanza kazi. Kadhalika, alisema kuwa Hayati Rais wa awamu ya tano John Magufuli, alikuwa amepanga serikali kununua meli za uvuvi nane kwa ajili ya Zanzibar na Tanzania Bara. Alisema wizara itasimamia kuhakikisha zinanunuliwa meli hizo nane mpya na zenye vifaa vyote kwa ajili ya uvuvi wa bahari kuu ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya uvuvi na kusafirisha nje ya nchi.

Pia alisema kipaumbele kingine itakuwa ni uboreshaji wa vituo vya uzalishaji wa vifaranga vya samaki ili kuhamasisha jamii kuanza ufugaji wa samaki katika maeneo yao.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alisema kuwa wameanzisha kampeni ya kuhamasisha jamii kuhusu ufugaji wa samaki na wanatarajia kuweka mashamba darasa katika kila wilaya nchini.

"Pia tunatarajia kufanya upembuzi yakinifu katika maeneo ya bahari na maziwa ili kubaini maeneo ambayo tunaweza kuwapatia wananchi wanaohitaji kufuga samaki katika vizimba kando ya maeneo hayo," alisema Ndaki.

# TASAF yawajengea zahanati wakazi Goima

**Na Renatha Msungu,** CHEMBA

WAJAWAZITO katika kijiji cha Igunga, Kata ya Goima, wilayani Chemba mkoani Dodoma, wameondokana na adha ya kutembea umbali wa kilomita saba kwenda kijiji cha Goima kupata huduma ya afya, baada ya Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF), kuwajengea zahanati.

Kijiji hicho chenye wakazi 3,600, awali walilazimika kutembea umbali wa kilomita saba kuelekea kituo cha afya cha Goima na Hamai kwa ajili ya kupata huduma za afya.

Mwenyetiki wa kijiji cha Igunga, Juma Bakari, alisema hayo juzi wakati wa ziara ya kutembelea wanufaika wa TASAF.

Bakari alisema, kabla ya TASAF kushirikiana na wakazi wa kijiji hicho kujenga

Scanned with CamScanner

# Dkt. Tamatamah: Utashi wa Hayati Magufuli chachu ya maendeleo sekta ya uvuvi

**Na Mbaraka Kambona, Morogoro**

KATIBU Mkuu,Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dkt. Rashid Tamatamah amesema kuwa utashi wa aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati, Dkt. John Magufuli wa kuamua kuwekeza katika Sekta ya Uvuvi umechangia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya sekta hiyo.

Dkt.Tamatamah alisema hayo alipokuwa akifungua warsha ya Uzinduzi wa Mpango Kazi wa Kutekeleza Mwongozo wa Hiari wa Uendelezaji wa Uvuvi Mdogo nchini inayofanyika mkoani Morogoro kuanzia Machi 30-31, 2021.

Akiongea na wadau wa Sekta ya uvuvi waliohudhuria warsha hiyo ya siku mbili, Dkt. Tamatamah alisema kuwa utayari wa Hayati Dkt. Magufuli kuwekeza katika sekta ya uvuvi umesababisha kuanzishwa kwa miradi mbalimbali ya maendeleo katika sekta hiyo.

"Sisi ambao tupo katika ngazi za juu za Wizara tunatambua kwamba utayari wake wa kuona kwamba mchango wa sekta ya uvuvi unakuwa mkubwa katika pato la Taifa umepelekea mipango mikubwa ya uwekezaji ambayo itatekelezwa wizarani katika mwaka ujao wa fedha," alisema Dkt. Tamatamah

Aliendelea kusema kuwa utayari wake wa kununua Meli nane (8) za kufanya uvuvi katika bahari kuu ulipelekea timu ya wataalamu wa Serikali iliyokuwa kwenye majadiliano na Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Kilimo (IFAD) kuhusu mkopo wa kuendeleza sekta ya uvuvi waweke kipaumbele ununuzi wa meli hizo miongoni mwa vitu vitakavyofadhiliwa na mradi huo.

"Katika mwaka ujao wa fedha 2021/22, Serikali itatumia kiasi cha shilingi Bilioni 50 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Bandari ya kwanza ya uvuvi ambao utafanyika katika eneo la Mbegani Bagamoyo, hizi zote ni juhudi na msukumo wake," alifafanua Dkt.Tamatamah.

Aidha,Dkt.Tamatamah alisema pamoja na nchi kupata msiba huo, uongozi uliopo sasa chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan hakuna shaka kuwa mipango yote ya uwekezaji iliyoachwa na Hayati, Dkt. Magufuli katika Sekta ya Uvuvi itatekelezwa kama ilivyopangwa ili kutimiza malengo yaliyowekwa katika utawala wake.

Kuhusu Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kutekeleza Mwongozo wa Hiari wa Uendelezaji wa Uvuvi Mdogo Nchini, Dkt.Tamatamah alisema kuzinduliwa kwa mpango huo kutakuwa ni ukombozi kwa wavuvi wadogo kwa sababu mwongozo huo umeweza kuonesha njia bora zitakazowezesha hali ya wavuvi wadogo kuimarika na kuinua uchumi wao.

"Mpango huu utasaidia wavuvi wadogo kufanya uvuvi endelevu ikiwemo kusimamia rasilimali za uvuvi katika muktadha wa chakula na kuondoa umasikini," alisema Dkt. Tamatamah

Kwa upande wa wadau,Katibu wa Kikundi cha Ulinzi Shirikishi cha Rasilimali za Bahari (BMU), Kilindoni, Wilayani Mafia alisema kuwa wanaishukuru serikali kutambua mchango wa wavuvi wadogo na kuamua kuandaa mpango huo ambao utawasaidia kupata masoko ya uhakika na zana bora za uvuvi kwa ajili ya uvuvi endelevu.

Naye, Suzana Ezekiel Mvuvi Mdogo anayefanya shughuli zake katika Mwalo wa Kibirizi, Kigoma alisema kuwa wavuvi wengi wadogo bado wanafanya shughuli zao kwa kubahatisha lakini Mpango kazi huo utawawezesha.




**Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dkt. Rashid Tamatamah akiongea na wadau wa uvuvi (hawapo pichani) wakati akifungua Warsha ya Uzinduzi wa Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kutekeleza Mwongozo wa Hiari wa Uendelezaji wa Uvuvi Mdogo Nchini ambapo alieleza kuwa Uvuvi mdogo una mchango mkubwa katika kuhakikisha usalama wa chakula na kuondoa umasikini hasa katika nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania.** (Na Mpigapicha Wetu)

Scanned with CamScanner

Aprili 1, 2021 Uk. 17, Habari Leo

# Uwekezaji katika uvuvi kuinua sekta

**Na Mwandishi Maalumu**

KATIBU Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dk Rashid Tamatamah amesema utashi wa Rais wa Awamu ya Tano,John Magufuli wa kuamua kuwekeza katika sekta ya uvuvi umechangia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya sekta hiyo.

Dk Tamatamah alisema hayo alipokuwa akifungua warsha ya uzinduzi wa Mpango Kazi wa Kutekeleza Mwongozo wa Hiyari wa Uendelezaji wa Uvuvi Mdogo nchini inayofanyika Mkoani Morogoro kuanzia Machi 30-31, 2021.

Alisema kuwa utayari wa Dk Magufuli kuwekeza katika sekta ya uvuvi umesababisha kuanzishwa kwa miradi mbalimbali ya maendeleo katika sekta hiyo.

Aliendelea kusema kuwa utayari wake wa kununua meli nane za kufanya uvuvi katika bahari kuu uliwezesha timu ya wataalamu wa Serikali iliyokuwa kwenye majadiliano na Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Kilimo (IFAD) kuhusu mkopo wa kuendeleza sekta ya uvuvi waweke kipaumbele ununuzi wa meli hizo miongoni mwa vitu vitakavyofadhiliwa na mradi huo.

"Katika mwaka ujao wa fedha 2021/22, Serikali itatumia kiasi cha shilingi Bilioni 50 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Bandari ya kwanza ya uvuvi ambao utafanyika katika eneo la Mbegani Bagamoyo, hizi zote ni juhudi na msukumo wake,"alifafanua Dk Tamatamah

Kuhusu Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kutekeleza Mwongozo wa Hiari wa Uendelezaji wa Uvuvi Mdogo Nchini, Dk Tamatamah alisema kuzinduliwa kwa mpango huo kutakuwa ni ukombozi kwa wavuvi wadogo.

"Mpango huu utasaidia wavuvi wadogo kufanya uvuvi endelevu ikiwemo kusimamia rasilimali za uvuvi katika muktadha wa chakula na kuondoa umasikini," alisema Dk Tamatamah

Katibu wa Kikundi cha Ulinzi Shirikishi cha Rasilimali za Bahari (BMU), Kilindoni, Wilayani Mafia alisema kuwa wanaishukuru serikali kutambua mchango wa wavuvi wadogo na kuamua kuandaa mpango huo ambao utawasaidia kupata masoko ya uhakika na zana bora za uvuvi kwa ajili ya uvuvi endelevu.

Suzana Ezekiel, Mvuvi Mdogo anayefanya shughuli zake katika Mwalo wa Kibirizi, Kigoma alisema kuwa wavuvi wengi wadogo bado wanafanya shughuli zao kwa kubahatisha lakini Mpango kazi huo utawawezesha kuondokana na hali hiyo na kufanya uvuvi endelevu na wa uhakika.

Scanned with CamScanner